**(IJA)**

**CHUO CHA UONGOZI WA MAHAKAMA**

**LUSHOTO**

# HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA, JAJI MKUU WA TANZANIA KATIKA MAHAFALI YA KUMI NA TISA (19) YA CHUO CHA UONGOZI WA MAHAKAMA LUSHOTO TAREHE 29 NOVEMBA, 2019 YALIYOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA NYALALI IJA - LUSHOTO

Mheshimiwa Jaji Dkt. Gerald Ndika, Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo na Jaji Mahakama ya Rufani;

Mheshimiwa Jaji Amir Mruma, Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu Kanda ya Tanga,

Mheshimiwa Jaji Dkt Fauz Twaib, Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu Kanda ya Moshi,

Mheshimiwa Jaji Dkt. Paul Faustin Kihwelo, Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto,

Mhe Mkuu wa Wilaya ya Lushoto,

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Uongozi wa Chuo;

Ndugu Viongozi wa Serikali, Taasisi za Dini na Vyama vya Siasa;

Wageni Walikwa;

Wahadhiri wa Chuo;

Ndugu Watumishi wa Chuo;

Ndugu Wazazi na Walezi wa Wahitimu;

Ndugu wanahabari;

Wahitimu wote waliosoma Chuo cha Uongozi wa Mahakama ambao wamehudhuria Mahafali ya leo;

Ndugu Wahitimu na Wanachuo Wote;

Mabibi na Mabwana.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza**, ninayo furaha isiyo kifani ya kuwa Mgeni Rasmi kwenye Mahafali ya Kumi na Tisa ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, hii ikiwa ni mahafali yangu ya pili kuhudhuria nikiwa mgeni rasmi.

Kwa dhati ya moyo wangu, nashukuru Baraza la Uongozi wa Chuo na kwako Mwenyekiti wa Baraza kwa kunipa mwaliko sio tu wa kuhudhuria lakini pia wa kuwa mgeni rasmi kwenye mahafali haya. Tangu nilipowasili hapa Chuoni nimekirimiwa kwa kiasi kikubwa na kujiona fahari ya kuwa ni sehemu ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. **Ninawashukuru sana kwa mapokezi na ukarimu wenu.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza**, nimesikiliza kwa makini hotuba yako pamoja na maelezo yaliyotolewa na Mkuu wa Chuo kuhusu maendeleo ya Chuo hiki, hususani utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2018/19-2022/23) kama Dira na muongozo wa masuala mbalimbali mnayosimamia. Ninapenda nichukue fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwako wewe binafsi, wajumbe wa Baraza la Uongozi wa Chuo na Menejimenti ya Chuo, kwa kukiongoza Chuo hiki pamoja na utekelezaji wa dhati wa malengo yake katika Mpango Mkakati wa Miaka Mitano.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza**, ninaomba nitamke kwa dhati kabisa kuwa natambua na kuthamini mchango na matunda ya Chuo hiki. Natambua kwamba toka kianzishwe, kimetoa wanafunzi mahiri ambao wameweza kufanya kazi mahakamani katika nafasi ya Usajili, Uhakimu na Ukarani. Watumishi hawa wamefanya kazi kwa weledi mkubwa na kuifanya mahakama kupata heshima stahiki kupitia utumishi wao. Aidha, lazima niseme kwamba, ni kutokana na utendaji wao mzuri wa kazi hata katika miaka hii ya karibuni Serikali iliamua kuwaajiri kama Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji. Mbali na nafasi hizo, natambua kwamba wahitimu wa Chuo hiki wamekuwa wakipata ajira katika taasisi mbalimbali za umma na binafsi kutokana na uadilifu na umahiri wa uchapaji kazi uliotokana na mafunzo wanayoyapata chuoni hapa. Mchango wa Chuo hiki katika Taifa hili

kupitia kwa wahitimu wake wanaofanya kazi sehemu mbalimbali nchini unafahamika na kutambuliwa vyema.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza**, katika hotuba yako umeeleza namna Chuo kinavyoendeleza watumishi wake kitaaluma. Ninafahamu kwamba Baraza la Chuo likishirikiana na Menejimenti ya Chuo limeweza kuwaendeleza watumishi wake, wanataaluma na waendeshaji. Hii inafanya kusiwepo mwanataaluma yeyote aliyebakia katika ngazi ya elimu ya Shahada ya kwanza na kwa watumishi waendeshaji wamekuwa wakiendelezwa katika ngazi mbalimbali katika maeneo yao. Nimeona pia katika Mpango Mkakati wa Chuo wa Miaka Mitano mmedhamiria kuwaendeleza watumishi waendeshaji katika ngazi za shahada ya kwanza, na wengine katika maeneo yao ili kuwajenga zaidi. Na kwa upande wa wanataaluma nimeona mna mpango wa kuwaendeleza wanataaluma wanne katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu. Nitumie fursa hii kuendelea kuwaomba muendelee kuwaendeleza wanataaluma pamoja na kada nyingine ili wanaporejea kazini waje na uwezo na weledi wa ziada kuweza kuipeperusha vizuri bendera ya Chuo pamoja na Mahakama.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza**, kuhusu mafunzo ya kozi fupi, ninatambua juhudi mnazofanya za kuendelea kutoa mafunzo endelevu ya kimahakama kwa wadau wa mahakama wakiwemo Wasambaza Nyaraka na Madalali wa Mahakama, na pia kwa watumishi wa Mahakama kama Majaji, Mahakimu na watumishi

wengine wa mahakama pamoja na wadau wengine wa sekta ya sheria. Hii itasaidia sana kuimarisha utendaji kazi wa wadau hawa muhimu wa mahakama ya Tanzania.

Ninapenda kuwahakikishia kwamba, Mahakama ya Tanzania imejipanga vyema kuitumia kikamilifu Kurugenzi ya Chuo hiki inayosimamia Mafunzo Endelevu ya Kimahakama. Ni muhimu ikaeleweka kwamba madhumuni ya msingi ya uanzishwaji wa Chuo ni kutoa mafunzo endelevu ya kimahakama kwa ajili ya kuwanoa kwa kuwapatia weledi stahiki watumishi wa Mahakama, ili wawe na ufanisi na ujuzi unaowawezesha kukabiliana na mabadiliko katika nyanja za kisheria, kiuchumi, kijamii na kiteknolojia.
Hii ni dhahiri kuwa Chuo hiki ni kitovu cha Mafunzo ya Kimahakama na Mafunzo Endelevu *(Judicial and Continuing Education)* nchini. Ninawasihi kuhakikisha kuwa mafanikio haya yanadumishwa.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza,** nimefurahishwa kwa namna ambayo Menejimenti ya Chuo inavyowajengea watumishi wake uwezo katika kufanya tafiti na kutoa huduma ya ushauri wa kitaalamu jambo lililopekea kupata mradi unaodhaminiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF)* wa kuwajengea uwezo watumishi wote wanaohusika na mashauri ya mtoto katika Mahakama zetu za Tanzania Bara. Nimefurahi sana kusikia kuwa mafunzo hayo yameendeshwa kwenye kanda zote za mahakama na mmejizatiti mtamalizia kanda mbili zilizobaki.

**Hongereni sana.** Mbali na mradi huo, nimefarijika pia kusikia kwamba Chuo kimepata mradi mwingine unaotekelezwa kwa pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (*FAO)* wa kutoa mafunzo kwa maafisa wanaoshughulikia na utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa njia mbadala. Hii inaonesha kwamba, Chuo kimeaminiwa na kujijengea heshima ya kutambuliwa mbele ya wadau wa maendeleo na niwaase kuendeleza juhudi zaidi ili kuweza kupata miradi mingi itakayosaidia kuwajengea uwezo watoa haki na hivyo kuboresha utendaji kazi wa mahakama pamoja na kupunguza mrundikano wa mashauri mahakamani.

Kuhusu machapisho nichukue fursa hii kuipongeza Menejimenti kwa kusimamia suala la uandaaji wa machapisho mbali mbali ikiwemo machapisho ya kufundishia watumishi wa mahakama wa ngazi mbalimbali na wadau wengine ambao wanafanya kazi kwa karibu na mahakama lakini pia kugharamia Jarida la Kitaaluma kila mwaka. Niseme tu kwamba, mimi ni mwanataaluma na ninajua changamoto za kufanya majarida kama haya kuwa endelevu, yaani kuchapisha kwa miaka mitatu mfululizo, ninawapongeza sana. Aidha, niwaase kuhakikisha kuwa juhudi hizi zinakuwa endelevu na kutokana na nafasi ya chuo hiki kwa mahakama niwaase muweze kuandika na kutunza historia za Majaji wastaafu pamoja na wale waliotangulia mbele ya haki kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho. Nafahamu kwa sasa Menejimenti imeanza uandishi wa kitabu cha Historia ya Marehemu Jaji Robert Herbert Kisanga, Jaji Mstaafu wa Mahakama

Rufaa na Mwenyekiti Mstaafu wa Tume ya Haki za Binaadam na Utawala Bora. Kazi hii inafanywa kufuatia maombi ya familia kwa mahakama hivo nina wapongeza kwa kukubalia kufanya kazi hii muhimu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza,** katika hotuba yako umeeleza namna ambavyo Chuo kinashiriki kutoa huduma za kijamii, hususani kutoa msaada wa kisheria kwa wenye uhitaji. Niendelee kuipongeza Menejimenti ya Chuo pamoja na watumishi wake na wahitimu wa chuo hiki kwa kazi waliyoifanya ya kutoa msaada wa kisheria bure kwa wananchi katika maeneo ya Korogwe, Bumbuli, Lushoto na Mlalo. Aidha, niendelee kuwaomba muendelee kuwasaidia wananchi na jamii inayowazunguka ili waone umuhimu wa Chuo hiki na kupata matunda yake. Waswahili husema ukiishi na waridi lazima unukie waridi. Muendelee kuimarisha Kitengo cha Msaada wa Kisheria ili wananchi wa Lushoto na maeneo ya jirani wafaidike na uwepo wake.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza,** napenda kukupongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza, pamoja na Menejimenti, kwa jitihada ambazo mnafanya kila siku za kuendeleza Chuo. Ninaahidi Mahakama ya Tanzania itaendelea kushirikiana pamoja na Baraza lako kukiendeleza Chuo hiki; kwa kuwahakikishia hili nawafahamisha kwamba muwe huru wakati wote kuja kwa ajili ya majadiliano kwenye Ofisi yangu, ya Mheshimiwa Jaji Kiongozi, Msajili Mkuu na vile vile ya Mtendaji

Mkuu wa Mahakama ili tuweze kutatua changamoto zinazotukabili na hatimaye tuweze kufikia lengo tulilolikusudia kwa kuwa sisi sote tunajenga nyumba moja na huwa tunajiona fahari pale Chuo chetu kinapofanya vizuri katika nyanja zote.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo,** moja ya matunda mazuri sana yanayozalishwa kila mwaka ni wahitimu. Kwa wahitimu wa leo, kwa miaka hii miwili na baadhi yenu mwaka mmoja mmekutana na changamoto mbalimbali katika safari yenu ya masomo na wengine mlioanza nao wamerudi nyumbani bila vyeti lakini ninyi mmeweza kuogelea katika bahari ya elimu na kuvuka kwa kushinda changamoto zote. Hii imetokana na kusoma kwa bidii na kushirikiana vizuri miongoni mwenu, wahadhiri na watumishi wengine wa Chuo.

Napenda nami nitumie fursa hii kuwapongeza wahitimu wetu wote ambao wamehitimu na watakaotunukiwa hivi punde Stashahada ya Sheria na Astashahada ya Sheria, niwapongezeni sana kwa kazi kubwa ya kutekeleza majukumu yenu ya kimasomo kwa muda wote mliokuwa hapa Chuoni. Kumbukeni mafanikio yenu hayatapimika tena kwa mitihani ya muhula, mawasilisho ya semina ama majaribio ya kuandika. Isipokuwa kwamba kila siku jamii itawapima ni kwa kiasi gani mnajitoa kwa ajili ya ustawi wa familia zenu na jamii kwa ujumla. Timizeni wajibu wenu mkikumbuka kauli mbiu ya Chuo ambayo ni Elimu, Haki na

Wajibu. Kumbukeni kuwa elimu yenu ni kwa faida ya huduma bora mtakayotoa popote mtakapokuwa.

Aidha, nami niungane na mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo kuwakumbusha silaha ya elimu ya sheria mliyoipata hamna budi kuitumia kikamilifu, kwa kuinoa kila wakati ili silaha hiyo iwe na nguvu ya kuibadilisha dunia. Katika fani ya sheria, moja ya njia ya kuinoa silaha hiyo ni kujisomea kila wakati kwa sababu sheria na kanuni huwa zinabadilika mara kwa mara. Sio vyeti vyenu vitakavyofanya kazi ya kutoa huduma. Kwa kuhitimu hivi leo haina maana kwamba mtakuwa mmemaliza kujifunza masuala yote ya kisheria, bali mnapaswa kuendelea kuwa wanafunzi kila wakati ili kujua sheria mpya na kanuni zake pindi zinapobadilika.

Mhitimu mzuri ni yule anayeacha milango wazi ya kujifunza kutoka kwa wengine.

Ninawaasa popote pale mtakapokuwa **JIFUNZENI** jambo jipya kila siku ili msipitwe na wakati na mkaiaibisha fani yenu, jiendelezeni hadi kufikia viwango vya juu kabisa katika fani hii muhimu.

Jengeni tabia ya kujisomea wenyewe vitabu ili kuendelea kujielimisha. Kamwe usimtegemee mtu mwingine asome kisha akuelekeze. Katika kujisomea, hakikisheni mnasoma pia mambo yasiyo ya kisheria kwa mfano hivi karibuni, Mhe. Benjamin William Mkapa (Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu) alizindua kitabu chake

“*My Life” My Purpose, A TANZANIA PRESIDENT REMBERS*” kitabu ambacho kitawaongezea ufahamu wa historia ya nchi yetu kupitia miaka 81 ya maisha ya Rais wa Awamu ya Tatu. Weledi, na maarifa na ujuzi mwingine haupatikani kupitia vyuoni bali kujisomea, kujiendeleza na kujifunza kutoka kwa wengine.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza,** wakati wa zoezi la uhakiki wa vyeti nchi nzima, Jaji Mkuu na viongozi wote wa Mahakama, pamoja na watumishi wote; tulitakiwa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama kuwasilisha vyeti vyetu halisi ili vihakikiwe na Baraza la Mitiani. Nilikuwa nje ya Dar es Salaam na niliomba nyumbani wafungue masanduku ya zamani kutafuta vyeti vyangu. Kuna wakati nilidhani vyeti vimepotea. Ilinichukua mimi na familia yangu zaidi ya wiki moja kuweza kufungua kila sanduku la zamani ili kuzipata zote na baadhi ya vyeti vilikuwa tayari zimebadilika hadi rangi.

Nilijifunza mambo mengi katika zoezi langu binafsi la kutafuta wapi vyeti vyangu vilipojificha! Kwanza, niligundua kuwa kazi za vyeti ni siku ya kuomba kazi tu. Baada ya kupata kazi kilicho muhimu sio vyeti tena, bali ni huduma, ujuzi na weledi wako ndio muhimu. Nilijifunza pia kuwa, unaweza kujisomea na kujiongezea maarifa na ujuzi ukawa ni bora zaidi ya kinachoeelezwa ndani ya vyeti. Hali kadhalika, wananchi na wenzako kazini wanaweza kupima huduma zako, ujuzi wako na weledi wako na kutathmini kuwa ni mbovu na hafifu kuliko kilichoandikwa katika vyeti vyako.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza,** naomba nitumie fursa hii pia kuwakumbusha wahitimu kwamba, taswira ya Chuo hiki imejengwa na wahitimu wenzenu waliowatangulia na kuwafanya ninyi mkapata habari njema juu ya Chuo hiki mkaja kujiunga kusoma. Kwasababu hiyo, popote mtakapokuwa, wale mtakaoenda kujiendeleza kwenye vyuo vya elimu ya juu mkafanye bidii katika kusoma ili kuvifanya vyuo hivyo viendelee kuvutiwa na wahitimu wanaotoka Chuo hiki. Na kwa wale mtakaobahatika kufanya kazi maeneo mbalimbali, fanyeni kazi kwa umahiri mkubwa na kwa maadili, na kwa wakati na kulinda daima maslahi ya umma wa Tanzania na hivyo kuendelea kubeba taswira nzuri ya Chuo ipasavyo. Heshima ya Chuo hiki itashuka sana endapo kutakuwa na taarifa kuwa wanafunzi waliosoma hapa wana ugonjwa wa kupenda rushwa au kutofanya kazi kwa weledi, au ni wavivu.

Aidha, nawaasa kwa nafasi zozote mtakazo kuwa nazo katika jamii, kuchukia na kuikimbia rushwa kama ugonjwa unaoweza kuliangamiza Taifa.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza,** upo msemo kwa lugha ya kiingereza *"Every end has a new beginning, and every beginning has an end."* Siku ya leo ni mwanzo wa maisha yenu mapya kama yalivyoboreshwa na Stashahada ya Sheria au Astashahada ya Sheria. Sasa ndio mwanzo wa kuthibitisha kuwa ufaulu unaoonyeshwa katika nakala ya vyeti vyenu ni uhalisia wa ustadi

wenu, ni uhalisia wa taaluma yanu na pia weledi wanu. Soko la ajira la zama za laeo haliangalii vyeti peke yake; ndio maana pamoja na kuwa na vyeti, bado waajiri siku hizi watataka kuwasaili na kuwapa mitihani katika maeneo ambayo hamjasomea. Vyeti vizuri peke yake havitoshi kama unatabia mbaya ya ugomvi, kupenda majungu na uvivu. Changamoto ambazo mtakumbana nazo huko nje ya geti la chuo hiki, hayatakuwa na majibu kutoka katika vyeti vyenu. Changamoto hizo zitatatuliwa kwa namna mtakavyotumia elimu yenu yote muliyonayo kwa kuchanganya na elimu mtakayopata kutokana na kushirikiana na watu wengine. Kuweni wenye unyenyekevu wa kuendelea kujifunza kutoka kwa wengine.

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza,** ninaomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kukushukuru tena kwa kunipa heshima hii ya kuwa Mgeni Rasmi katika Mahafali haya ya Kumi na Tisa ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Nichukue nafasi hii kuwashukuru wazazi wenu, walezi wenu, ndugu na marafiki zenu ambao ni sehemu ya mafanikio yenu.

Mwisho, nawatakia kila la heri ninyi wahitimu na wageni waalikwa; tafadhali msherehekee kwa amani.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

***IJUMAA, NOVEMBA 29, 2019***